TANGAZO LA SERIKALI NA. 258 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya abiria;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ikiwa ni pamoja na maeneo ya

taasisi ya umma au watu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

“madini ya ujenzi” maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

“maegesho” maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada” maana yake soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

“mnunuzi wa mazao” maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika linalonunua mazao kwa ajili ya biashara au matumizi mengineyo katika eneo la Halmashauri;

“muuzaji wa mazao” maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika anayeuza au anayesafirisha mazao kutoka kata moja kwenda kata nyingine au nje ya eneo la Halmashauri mwenye mazao yenye uzito wa zaidi ya tani moja;

“soko” maana yake ni ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

“ushuru” maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

“ushuru wa huduma” maana yake ni ushuru unaotozwa au unaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la

Halmashauri;

"ushuru wa madini ya ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa kokoto, mawe, changarawe, mchanga, marumaru, kifusi, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi ikijumuisha tozo kwa mtu yeyote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine;

"utamaduni" maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, ususi, michezo, muziki wa dansi, video, muziki wa taarabu,maonyesho ya sinema, mazingaombwe,tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kadiri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada au

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru

ushuru

kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ushuru wa huduma

7.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao hawawasilishi hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(3) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara anawajibu wa kulipa ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa za hesabu za mwaka kwa ajili ya kukokotoa kiwango.

(4) Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa ushuru wa huduma katika kipindi maalumu cha hesabu.

(5) Kila mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa ushuru wa huduma ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo za (3) na (4), Mkurugenzi wa Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na

uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya suala lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Kamati ya mapato

11.-(1) Kutakuwa na Kamati yakufuatilia mapato ya Halmashauri itakayoundwa na Mkurugenzi ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu utendaji kazi wa kikosi kazi cha kukusanya mapato;

(b) kuishauri Halmashauri kuhusu namna ya kuongeza mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato;

(c) kufanya tathimini ya makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka ili kuweka maoteo ya mwaka unaofuata.

(2) Kamati ya mapato itawajibika kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa Menejimenti kila mwezi kuonesha

namna ilivyofanya kazi katika kipindi husika.

Kikosi kazi cha kudhibiti mapato

12.-(1) Kutakuwa na kikosi kazi cha kufuatilia na kudhibiti utoroshaji wa mapato ambacho kitaundwa na Mkurugenzi kikihusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali za Halmashauri.

(2) Kikosi kazi kitakachoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kitawajibika kwa Kamati ya Mapato.

Makosa

13. Mtu yeyote-

(a) atakayeshindwa, dharau, kwepa au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atakayemshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atakayemzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atakayetumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) atakayetoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; na

(f) atakayetumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada,

anatenda kosa.

Adhabu

14. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

**1.** Ada ya kukodi mali za Halmashauri.

| Na | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri | 100,000/= kwa siku. |
| 2. | Kukodi viti | 300/= kwa kila kiti kwa siku. |
| 3. | Kukodi meza | 500/= kwa kila meza kwa siku. |
| 4. | Lori | 50,000/= kwa tripu.<br>Mafuta ni juu ya mkodishaji. |
| 5. | Mziki/Vipaza sauti | 80,000/= kwa siku |
| 6. | Mgahawa | 100,000/= kwa Mwezi |

**2.** Ada ya ushuru wa mazao ya kilimo, biashara na chakula

| Na. | Aina ya mazao. | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Miwa | 3% ya bei ya kununulia. |
| 2. | Pamba | 3% ya bei ya kununulia |
| 3. | Kahawa | 3% ya bei ya kununulia |
| 4. | Maharage | 3% ya bei ya kununulia |
| 5. | Mpunga | 3% ya bei ya kununulia |
| 6. | Mahindi | 3% ya bei ya kununulia |
| 7. | Alizeti | 3% ya bei ya kununulia |
| 8. | Karanga | 3% ya bei ya kununulia |
| 9. | Vitunguu | 3% ya bei ya kununulia |
| 10. | Mtama | 3% ya bei ya kununulia |
| 11. | Viazi mviringo | 3% ya bei ya kununulia |
| 12. | Magimbi | 3% ya bei ya kununulia |
| 13. | Ndizi | 3% ya bei ya kununulia |
| 14. | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Mihogo | 3% ya bei ya kununulia |
| 16. | Mchele | 3% ya bei ya kununulia |
| 17. | Korosho | 3% ya bei ya kununulia |
| 18. | Tumbaku | 3% ya bei ya kununulia |
| 19. | Ufuta | 3% ya bei ya kununulia |
| 20. | Mbaazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 21. | Soya | 3% ya bei ya kununulia |
| 22. | Mazao mengineyo ya Chakula | 2% ya bei ya kununulia |
| 23. | Mazao mengineyo ya Biashara | 3% ya bei ya kununulia |

**3.** Ada ya Huduma za ukaguzi wa nyama

| Na. | Aina ya mfugo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ng`ombe | 2,500/= kila mmoja |
| 2. | Mbuzi | 1,000/= kila mmoja |
| 3. | Kondoo | 1,000/= kila mmoja |
| 4. | Nguruwe | 1,000/= kila mmoja |
| 5. | Kuku | 200/= kila mmoja |

**4.** Ada ya Huduma za Machinjio

| Na. | Aina ya mfugo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ng`ombe | 2,500/= kila mmoja |
| 2. | Mbuzi | 1,000/= kila mmoja |
| 3. | Kondoo | 1,000/= kila mmoja |
| 4. | Nguruwe | 1,000/= kila mmoja |
| 5. | Kuku | 200/= kila mmoja |

**5.** Ada ya Ukaguzi wa afya.

| Na | Aina ya shughuri | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Kupimwa afya kwa wahudumu wa nyumba za kulala wageni, hoteli, migahawa, wauzaji wa bucha ya nyama. | 5,000/= kwa kila mmoja kila baada ya miezi sita. |
| 2. | Kupimwa afya kwa wahudumu wa Baa, Glocery na vilabu vya pombe za kienyeji. | 5,000/= kwa kila mmoja kila baada ya miezi sita. |

**6.** Ushuru wa maegesho

| Na. | Chombo cha usafiri | Kiwango. |
|---|---|---|
| 1. | Gari la mizigo zaidi ya tani 7. | 5,000/= kwa siku |
| 2. | Gari la mizigo chini ya tani 7 | 3,000/= kwa siku |
| 3. | Magari mengine yasiyo na biashara | 1000/= kwa siku |
| 4. | Mabasi makubwa | 2,000/= kwa siku |
| 5. | Mabasi madogo | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Tax | 500/= kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na. 268 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Pikipiki na Bajaji | 500/= kwa siku |
| 8. | Magari yanayoegeshwa maeneo ambayo hayaja ruhusiwa | 5,000/= kwa kila gari moja |

**7.** Ushuru wa stendi

| Na | Chombo cha usafiri | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa ya abiria sitini na kuendelea | 2,000/= |
| 2. | Mabasi madogo ya abiria chini ya abiria sitini | 1,000/= |
| 3. | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/= |
| 4. | Tax | 500/= |
| 5. | Pikipiki na Bajaji | 500/= |
| 6. | Ada ya kutunza gari lilokamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= kwa kila siku |
| 7. | Mtu asiye na tiketi ya safari au ya kuingia, kutoka eneo la ndani ya stendi | 200/= |

**8.** Ushuru wa madini ya ujenzi

| Na | Aina ya madini | Uzito wa gari | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchanga | Chini ya tani 7<br>Tani 7 hadi 10<br>Zaidi ya tani 10 | 2,000/= kwa tripu moja<br>4,000/= kwa tripu moja<br>5,000/= kwa tripu moja |
| 2. | Mawe | Chini ya tani 7<br>Tani 7 hadi 10<br>Zaidi ya tani 10 | 2,000/= kwa tripu moja<br>4,000/= kwa tripu moja<br>5,000/= kwa tripu moja |
| 3. | Kifusi | Chini ya tani 7<br>Tani 7 hadi 10<br>Zaidi ya tani 10 | 2,000/= kwa tripu moja<br>4,000/= kwa tripu moja<br>5,000/= kwa tripu moja |
| 4. | Udongo | Chini ya tani 7<br>Tani 7 hadi 10<br>Zaidi ya tani 10 | 2,000/= kwa tripu moja<br>4,000/= kwa tripu moja<br>5,000/= kwa tripu moja |
| 5. | Ada ya ukaguzi wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi | - | 30,000/= |
| 6. | Ada ya umiliki wa eneo la kuchimbwa madini ya ujenzi | - | 100,000/= kwa mwaka |
| 7. | Madini ya dhahabu, alimasi, makaa ya mawe, vito, ulanga, chuma, jipsam, na madini mengineyo | | 500,000/= kwa mwaka |

**9.** Ada ya uzoaji taka

| Na. | Eneo | Kiwango |
|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na. 268 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Baa, hoteli, Taasisi, Mgahawa | 3,000/= kwa mwezi |
| 2. | Duka | 2,000/= kwa mwezi |
| 3. | Nyumba ya kuishi | 500/= kwa mwezi |
| 4. | Nyumba ya kulala wageni | 2,000/= kwa mwezi |

**10.** Ushuru wa matangazo

| Na | Maelezo | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kufanya matangazo | 2,000/= kwa matangazo ya siku moja |
| 2. | Matangazo kwenye mabango yanayo ng`aa na yasiyozidi sqft2<br>Matangazo kwenye mabango yanayo ng`aa yanayozidi sqft2 | 15,000/= kwa mwaka<br>25,000/= kwa mwaka |
| 3. | Matangazo kwenye mabango yasiyo ng`aa yasiyozidi sqft2<br>Matangazo kwenye mabango yasiyo ng`aa yanayozidi sqft2 | 8,000/= kwa mwaka<br>10,000/= kwa mwaka |
| 4. | Matangazo kwa kutumia vipaza sauti na magari, promosheni maeneo ya wazi, | 20,000/= kwa siku |

**11.** Ushuru wa shughuli za utamaduni na sanaa

| Na | Maelezo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kibali cha kufanya sanaa za maonyesho ya utamadun/kumbi za video. | 10,000/= kwa kila onyesho/tukio. |
| 2. | Maombi ya kibali cha kupigisha dansi na muziki. | 10,000/= kwa siku.<br>100,000/= kwa mwaka. |
| 3. | Maombi ya kibali cha kufanya tiba za jadi. | 30,000/= kwa mwaka |

**12.** Ushuru wa mazao ya misitu

| Na | Aina ya zao | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 500/= kwa gunia |
| 2. | Mbao | 500/= kila ubao |
| 3. | Kuni | 500/= kila mita moja ya ujazo |
| 4. | Nguzo | 500/= kila nguzo |
| 5. | Gogo | 3,000 /= kila mita ya ujazo |
| 6. | Fito | 1,000/= kila mita ya ujazo |
| 7. | Asali | 100/= kila lita moja |
| 8. | Nta | 100/= kila lita moja |

**13.** Ada ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi

| Na. | Maelezo | Kiasi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Makazi kuwa biashara | 20,000/= |
| 2. | Biashara kuwa viwanda | 20,000/= |
| 3. | Kugawanya viwanja au shamba | 25,000/= |
| 4. | Kuhakiki miliki | 25,000/= |

**14.** Ushuru wa minada ya Mifugo na usafirishaji wake

| Na | Aina ya Mifugo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ng`ombe | 4,000/= kwa kila mfugo alieuzwa |
| 2. | Mbuzi, Kondoo, Nguruwe. | 1,000/= kwa kila mfugo alieuzwa |

**15.** Ada ya unyonyaji maji machafu

| Na | Eneo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Eneo la biashara | 80,000/= kwa tripu moja |
| 2. | Eneo la makazi | 60,000/= kwa tripu moja |

**16.** Ushuru wa Huduma kwa Wafanyabiashara wasiofunga Hesabu za Biashara

| Na. | Kiwango cha Ada ya Leseni ya Biashara | Kiasi cha Ushuru wa Huduma kwa Mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Shilingi 5,000 hadi Shilingi 50,000 | 10,000 |
| 2. | Shilingi 51,000 hadi Shilingi 100,000 | 15,000 |
| 3. | Shilingi 101,000 hadi Shilingi 150,000 | 20,000 |
| 4. | Shilingi 151,000 hadi Shilingi 200,000 | 25,000 |
| 5. | Shilingi 201,000 hadi Shilingi 250,000 | 30,000 |
| 6. | Shilingi 251,000 hadi Shilingi 300,000 | 35,000 |
| 7. | Shilingi 301,000 hadi Shilingi 350,000 | 40,000 |
| 8. | Shilingi 351,000 hadi Shilingi 400,000 | 45,000 |
| 9. | Shilingi 401,000 hadi Shilingi 450,000 | 50,000 |
| 10. | Shilingi 451,000 hadi Shilingi 500,000 | 55,000 |
| 11. | Shilingi 501,000 hadi Shilingi 550,000 | 60,000 |
| 12. | Shilingi 551,000 hadi Shilingi 600,000 | 65,000 |
| 13. | Shilingi 601,000 hadi Shilingi 650,000 | 70,000 |
| 14. | Shilingi 651,000 hadi Shilingi 700,000 | 75,000 |
| 15. | Shilingi 701,000 hadi Shilingi 750,000 | 80,000 |
| 16. | Shilingi 751,000 hadi Shilingi 800,000 | 85,000 |
| 17. | Shilingi 801,000 hadi Shilingi 850,000 | 90,000 |
| 18. | Shilingi 851,000 hadi Shilingi 900,000 | 95,000 |
| 19. | Shilingi 901,000 hadi Shilingi 950,000 | 100,000 |
| 20. | Shilingi 951,000 hadi Shilingi 1,000,000 | 150,000 |
| 21. | Zaidi ya Shilingi 1,000,000 | 200,000 |

______________

__________

JEDWALI LA PILI

______________

___________________

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 15)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Namtumbo, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………….ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:

Jina:…………………………………..…………………….....
Saini………………………..………………………..………
Wadhifa: ………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Namtumbo ulioitishwa na kufanyika Tarehe 10 Mwezi Juni Mwaka 2022 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya;-

CHIRIKU HAMISI CHILUMBA
*Mkurugenzi Mtandaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo*

JUMA ALFAN PANDU
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo*

**L.S**

NAKUBALI

Dodoma,
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*